**Tobias Otieno Ayayo, (1928 – 2013)**

Tobias Otieno Ayayo ni mchungaji, mwalimu, mwinjilisti, na mmishionari kutoka nchi ya Kenya.

**Maisha ya Awali na Elimu**

Tobias Otieno Ayayo alizaliwa mnamo Novemba 11, 1928 katika kijiji cha Magunda, ambayo kwa sasa ni Kitongoji cha Malanga huko North Gem, Kaunti ya Siaya, Kenya, kwa Mchungaji Silfano Ayayo Mijema na Asenath Ngalo, binti ya Owiti Ongwana. Baba yake alichangia pakubwa katika kuleta Kanisa la Waadventista wa Sabato katika Central Kavirondo (ambayo baadaye ilikuja kuwa Central Nyanza na ambayo kwa sasa ni kaunti za Kisumu na Siaya).

Tobias Otieno Ayayo alitumia maisha yake ya utotoni huko Gem katika Kaunti ya Siaya, na ujana wake katika vituo mbalimbali vya Nyanza Kusini (kaunti za Homabay na Migori kwa sasa) ambako baba yake alifanyia kazi. Alipata elimu yake ya awali katika Shule ya Sekta ya Malanga kuanzia 1935 – 1937 kabla ya kuhamia Shule ya Sekta ya Maliera kuanzia 1938-1940. Kisha alihamia Shule ya Msingi ya Maliera kuanzia 1941 – 1944 na hatimaye Shule ya Msingi ya Rabwao mnamo 1945.

Kuanzia 1946 – 1948, alihudhuria Shule ya Kati ya Kamagambo ambako alibatizwa na Mchungaji Nicolao Opiyo mwaka wa 1946. Kuanzia 1949 – 1951, Ayayo alihudhuria Chuo cha Misheni cha Waadventista cha Bugema kwa mafunzo ya uchungaji. Aliporudi, akawa mwalimu na akapangwa Shule ya Msingi ya Nyamome na baadaye akahamia Shule ya Msingi ya Ranen. Kuanzia 1953 – 1954, alirudi Chuo cha Misheni cha Waadventista cha Bugema kusomea Teolojia.

**Familia**

Mnamo Machi 11 mwaka 1954, Mchungaji Tobias Otieno Ayayo alimuoa Rosebella Njoga, bintiye William Ayodo na Drusilla Sabwala. Watoto wa Rosebella ni pamoja na Samuel Onyango, Jonathan Onunga, Ezra Otieno, Modekai Osano, Ludiah Ojwang Okech, Mical Ndonga Omom, Hulda Abongo Oyugi na Judith Auma Okoyo, Damaris Osuri Ochola, na Caren Atieno Adhaya.

Tobias na Rosebella Otieno walibarikiwa na watoto wafuatao: Edwina Atieno, Stephen Ochieng, Zachary Ngalo, Paul Oluoch, Cleveland Ayayo, Christine Adhiambo, James Ayodo, na Rena Awino. Mama yake Tobias alifariki mnamo 1959, na baba yake alifariki mnamo Aprili 21, 1984.

**Uchungaji**

Alipomaliza Mafunzo yake ya Theolojia, Mchungaji Tobias Otieno Ayayo alianza kufanya kazi kama mhubiri na mwinjilisti. Kuanzia 1956 – 1960, alikuwa Chapleni katika Hospitali ya Misheni ya Kendu. Mnamo 1960, aliwekewa mikono ya uchungaji

na kutumwa katika Mtaa wa Lala chini ya Wiobiero Station kama mchungaji aliyewekewa mikono. Kuanzia 1961 – 1962 alifundisha katika Idara ya Kichungaji ya Chuo cha Misheni cha Bugema baada ya kuwa mchungaji aliyewekwa mikono. Kuanzia 1963 -1966, alihudumu kama mmishonari huko Tanganyika. Wito wake wa kwanza ulikuwa Dar-es-salaam, ambapo juhudi yake ya kwanza ilizalisha waongofu 27 ambao hatimaye walibatizwa. Idadi iliongezeka, na baadaye makanisa yalipandwa, misheni ilianzishwa, na fildi zikajengwa Dar-es-salaam, Kahama, Malampaka, Ntusi, na Bupandaghila katika eneo la Usukumani, na katika mikoa ya Bukoba na Geita. Mnamo 1967, alirudi Kenya na akapangwa kuhudumu huko Gwasi kama kiongozi wa mtaa. Gwasi kwa sasa ipo katika Kaunti ya Homabay.

**Kwenye Fildi ya Ranen**

Kati ya 1968 -1974, alifanya kazi kwenye Fildi ya Ranen kama mchungaji aliyewekewa mikono, afisa katika Elimu, Kiasi na YPMV, Utawala na Elimu, Kiasi na YPMV, Katibu wa Idara. Kama sehemu ya huduma yake, aliandaa kongamano la muziki la fildi ya Ranen. Kuanzia 1975 – 1989, alihudumu kama kiongozi wa mtaa katika mitaa ifuatayo: Karungu, Obera (Kabuoch), Sota (Kadem), Raguda (Karungu ), Migori Town, na Nyaduon'g.

Kati ya 1990 na 1992, alipangwa kufanya kazi katika Makao Makuu ya Ranen Field ambako alihudumu katika Kamati Tendaji ya Konferensi na katika Idara ya Shule ya Sabato, Uwakili, na Maendeleo, pamoja na majukumu yake ya kihuduma kama mhudumu aliyewekewa mikono. Ni katika kipindi hiki ambapo aliandaa uchangishaji fedha kupitia udugu wa Kanisa, Jumuiya, na marafiki wa Kanisa ambapo fedha zilizokusanywa ziliwezesha kufanyika yafuatayo. Jengo la maabara lilijengwa kwenye Shule ya Sekondari ya Ranen, gari la wagonjwa lilinunuliwa kwenye Kituo cha Afya cha Ranen, na nyumba kwa ajili ya wafanyakazi wawili wa fildi ya Ranen zilijengwa.

**Kustaafu**

Mnamo 1992, Mchungaji Tobias Otieno Ayayo alistaafu kutoka kwenye ajira ya kazi ya kanisa na kukaa nyumbani kwake Got Kayayo huko Achuth, Kaunti ya Migori, ambapo alianza awamu mpya ya maisha yake. Alianza utumishi wenye nguvu zaidi kwa Mungu na kwa wanadamu. Alichaguliwa kuhudumu katika bodi za Usimamizi (zamani Bodi ya Magavana) ya shule kadhaa na jumuiya yake.

Ayayo alipanga kuchangisha pesa ambapo rasilimali za kutosha zilihamasishwa na kuchangishwa ili kujenga Kanisa la Waadventista Wasabato la Got Kayayo likiwa na kisima cha ubatizo kilichokamilika na Kanisa hilo kuwekwa wakfu Julai 31, 2011. Ayayo alikuwa ametoa ardhi ambayo kanisa hilo lilijengwa. Kanisa la Maliera Central Seventh-day Adventist Church lilijengwa kwenye ardhi ambayo hapo awali ilikuwa makazi yao kabla ya wao kuhamia Nyanza Kusini. Baba yake alitoa shamba lote kwa kanisa. Kikawa Kituo cha Misheni cha Waadventista Wasabato. Kwenye ardhi hiyo

kwa sasa pamejengwa shule ya chekechea na shule ya msingi pamoja na Zahanati ya Waadventista Wasabato Maliera.

Kanisa la Waadventista Wasabato Magunda katika Kaunti Ndogo ya Gem ya Kaunti ya Siaya liko mahali alipozaliwa Magunda. Baada ya kuugua kwa muda mrefu, Tobias Otieno Ayayo aliaga dunia Julai 25, 2013 akiwa na umri wa miaka 84, katika Hospitali ya Jumuiya ya Jeremic huko Baraton nchini Kenya.